

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA SINGIDA.  
Anwani ya Simu: "MKUU MKOA"  
Simu Na.:2502170/2502089/2502249  
Nukushi Na. 2502078  
Barua pepe: ras.singida@tamisemi.go.tz  
ras@singida.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA,  
S. L. P. 5,  
SINGIDA.

### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI.

Mkuu wa Mkoa wa Singida Mheshimiwa Mhandisi Mathew J. Mtigumwe leo amekagua ujenzi wa daraja la sibiti linalounganisha Mikoa ya Singida na Simiyu ili kuona utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Dkt. John P. Magufuli la Julai 30, 2016 alipofanya ziara Mkoani Singida na kumtaka mkandarasi kuendelea na ujenzi wa daraja hilo mara moja.


Mheshimiwa Mhandisi Mtigumwe ameridhishwa na kasi ya ujenzi wa daraja hilo ambalo ujenzi wake umeanza tena mwezi Septemba 2016 baada ya kusimama kwa muda wa miezi 30 na linatarajiwa kukamilika Disemba 2017 pamoja na barabara za maungio ya daraja hilo zenye urefu wa kilomita 20, ambapo Mheshimiwa Rais alisema endapo Mkandarasi huyo atashindwa kuendelea serikali itateua mkandarasi mwingine.

Mheshimiwa Mhandisi Mtigumwe amesema daraja hilo ni muhimu kwa maendeleo ya wananchi wa mikoa ya Simiyu na Singida pamoja na mikoa ya kanda ya ziwa kutokana na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na watu na hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Wakati huohuo Mheshimiwa Mhandisi Mtigumwe ameagiza kukamatwa kwa Musoma Jimolas mkazi wa Meatu aliyejamilikisha njia ya dharura inayopita katikati ya daraja la sibiti licha ya kukatazwa na viongozi kadhaa akiwemo waziri wa ujenzi, uchukuzi na mawasiliano Profesa Makame Mbarawa, aidha amempiga marufuku kibarua wake Maduhu Tungungusa mkazi wa Ibaga kuwatoza kiasi cha shilingi elfu tano hadi elfu mbili watumiaji wa njia hiyo.

Daraja la Sibiti lina urefu wa mita 82 na upana wa mita 10.5 linajengwa na Mkandarasi wa kampuni ya kutoka China ya Hainan International Limited.

**Imetolewa na;**



Grace Gwamagobe

Afisa Habari

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

**SINGIDA.**

Novemba 8, 2016.